



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 07 Juni, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka 2024/2025.

Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii. Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii. Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka 2024/2025.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

62. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na changamoto ya kutupa taka ovyo katika njia iendayo Kisamakani katika shehia ya Tazari, jimbo la Nungwi. Taka hizi za mahoteli zinaathiri afya ya binaadamu waendao makondeni.

- (a) Je, ni nani hasa anaepaswa kukataza vitendo hivi ambavyo

vinaathiri afya za binaadamu.

- (b) Je, Wizara yako inatoa tamko gani juu ya wamiliki wa mahotelii haya.
- (c) Je, ni mikakati gani inayochukuliwa na Serikali juu ya kuzuia utupaji wa taka katika njia iendayo Kisamakani.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

203. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:
- (a) Ni tafiti ngapi na zipi zimefanyika kuhuisha kilimo hai nchini.
 - (b) Ni yepi matokeo ya tafiti hizo katika kuendeleza kilimo hai nchini.
 - (c) Je, Zanzibar tuna mashamba darasa mangapi yanayojihusisha na kilimo hai kwa sasa.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

30. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaipongeza Serikali kuititia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa hatua inazoendelea nazo za kuwaajiri walimu katika skuli mbali mbali visiwani Zanzibar. Hata hivyo, bado kuna changamoto ya upungufu mkubwa wa walimu katika skuli zetu hasa skuli ya Unguja Ukuu Msingi ambapo hadi kufikia mwezi Januari 2024, skuli hii ina jumla ya walimu 23 tu, ambao wanajukumu la kutoa taaluma kwa takriban wanafunzi 132, hali inayowapa wakati mgumu walimu hao katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

- (a) Je, Serikali hadi sasa ina mpango gani wa kuongeza idadi ya walimu katika skuli hii.
- (b) Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kuititia Wizara yako imelenga kuajiri walimu wangapi kwa skuli za msingi na hadi sasa ni walimu wangapi tayari wameshaajiriwa.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

172. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:
- (a) Kwa kiasi gani makosa mbali mbali yanayofanyika kwenye mitandao ya kijamii yanashughulikiwa ipasavyo.
 - (b) Ni kesi ngapi za makosa ya kimtandao zimeripotiwa na kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu ya sheria.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

128. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kuongezeka kwa utalii Zanzibar pamoja na athari nyengine, kumepelekea kuongezeka kwa watu kuzibadilisha nyumba zao za makaazi na kuwa nyumba za kulala wageni (Airbnb). Pamoja na kuwa jambo hili hupelekea kipato kizuri kwa wananchi, lakini limekuwa halina utaratibu mzuri na hupelekea malalamiko kwa wageni.

- (a) Je, ni upi utaratibu rasmi wa kubadilisha nyumba za makaazi na kuwa nyumba za kulala wageni (Airbnb).
- (b) Je, tathmini inaonyesha ni nyumba ngapi zimebadilishwa kutoka nyumba za makaazi na kuwa nyumba za kulala wageni (Airbnb).
- (c) Je, Serikali hupata mapato ya kiasi gani kwa mwaka, yanayotokana na nyumba hizi zilizobadilishwa kuwa za kulala wageni.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka 2024/2025.



(Raya Issa Msellel)
KATIBU WA BARAZA

Zanzibar,
07 Juni, 2024.